**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**WILAYA YA KIGAMBONI**

# RISALA YA UTII KWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA; MHESHIMIWA DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI INAYOSOMWA KWENYE SHEREHE ZA MBIO ZA MWENGE WA UHURU WILAYA YA KIGAMBONI TAREHE 28 MEI, 2017

**Imetayarishwa:**
**Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni,**
**S.L.P. 36124,**
**SIMU: +25522-2928474 ,**
**DAR ES SALAAM.**

**RISALA YA UTII KWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHESHIMIWA DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI INAYOSOMWA KWENYE SHEREHE ZA MBIO ZA MWENGE WA UHURU WILAYA YA KIGAMBONI TAREHE 28 MEI, 2017**

**Mheshimiwa Rais,**
Nachukua fursa hii kwa niaba ya viongozi na wananchi wote wa Wilaya ya Kigamboni, kukupongeza wewe na wote wanaokusaidia kusukuma mbele gurudumu la maendeleo vizuri na kwa umakini. Sote tunayaona mafanikio makubwa ya maendeleo ya nchi yetu ya kiuchumi, kijamii na utamaduni. Sisi wananchi wa Kigamboni tunakupongeza sana na tunaahidi kuendelea kukupa ushirikiano.
Aidha, tunawapongeza vijana wetu shupavu na wazalendo kwa kuuongoza na kuukimbiza Mwenge wa Uhuru katika nchi yetu. Tunatambua ugumu na uzito wa kazi hii lakini tunaamini wameifanya kazi hii na wataendelea kuifanya kwa uadilifu uliotukuka na uvumilivu mkubwa. Tunawakaribisha sana Kigamboni na mjisikie mko nyumbani.

**Mheshimiwa Rais,**
Wilaya ya Kigamboni ni miongoni mwa Wilaya tano za Mkoa wa Dar es salaam yenye ukubwa wa kilometa za mraba **416** ikiwa na Tarafa **1**, Kata **9** na mitaa **67** yenye wakazi **162,932** kulingana na Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012. Kufikia mwaka 2016 Wilaya ya Kigamboni inakisiwa kuwa na jumla ya wakazi **205,966** kutokana na ongezeko la watu la **5.6%** kwa mwaka.

**Mheshimiwa Rais**,
Uchumi wa Wilaya ya Kigamboni unategemea shughuli za kilimo, Uvuvi, viwanda na biashara. Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, asilimia **70** ya wakazi Kigamboni wamejiajiri na na asilimia **30** wameajiriwa katika sekta rasmi.

**Mheshimiwa Rais**,

Wilaya ya Kigamboni ina shule za Msingi **42.** Kati ya hizo **31**ni za Serikali na **11** zisizo za Serikali. Shule hizo zina wanafunzi **11,333** ambapo kati ya hao ni wavulana ni **5,762** na wasichana ni **5,571**.

Jumla ya walimu waliopo ni **578.** Vyumba vya madarasa vilivyopo ni 281 na madawati **9,240.**

Wilaya ya Kigamboni ina jumla ya shule za Sekondari **20.** Kati ya hizo shule **14** ni za Serikali na **6** zisizo za Serikali. Shule Hizi zina jumla ya wanafunzi **8,658.** Kati ya hao, wavulana ni **4,498** na wasichana **4,160**. Wilaya ya Kigamboni haina upungufu wa vyumba vya madarasa na madawati hasa kwenye shule zetu za Serikali.

**Mheshimiwa Rais,**

Hatua za kujenga na kuboresha miundombinu zimezingatiwa katika mwaka wa fedha 2016/2017. Halmashauri imeanza ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita **1.3** kwa kiwango cha lami na kilomita **25.3** kiwango cha changarawe, kujenga kalvati na mitaro ili kurahisha mawasiliano na uchukuzi na kukuza shughuli za kiuchumi katika Wilaya.

**Mheshimiwa Rais,**

Vyama vya Ushirika vya akiba na mikopo (SACCOS) vipo **11** vikiwa na wanachama **1,103**, akiba ya shilingi **2,939,890,300** na hisa **180,253,000**. Mikopo iliyotolewa na vyama hivyo hadi mwezi Machi 2017 ni **4,320,089,900**.

**Mheshimiwa Rais,**

Wilaya ya Kigamboni imepiga hatua kubwa katika uwezeshaji wa vijana. Wilaya ya Kigamboni ina vikundi **56** vya vijana vya uzalishaji mali vyenye wanachama **280** katika Kata **9.** Kati ya vikundi hivyo, vikundi **56** vinatoa ajira kwa vijana **280 (Kiambatisho I)**. Aidha, wilaya imetenga maeneo yenye jumla ya mita 25,200 za mraba katika Kata za Kigamboni, Mjimwema Tungi na Somangila kwa ajili ya vijana kufanyia biashara zao.

**Mheshimiwa Rais,**

Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni imetenga shilingi **493,842,261** ambayo ni asilimia **10%** ya mapato yake ya ndani ili kuwawezesha wanawake na vijana, ambapo wanawake wanatengewa asilimia **5%** na vijana asilimia **5%**. Vikundi **220** vya wanawake na vijana vimenufaika na mikopo hiyo ambapo **Tshs 254,050,000** zimekopeshwa kupitia benki ya DCB hadi sasa. Mikopo inaendelea kutolewa.

**Mheshimiwa Rais**,

Katika mapambano dhidi ya rushwa, tumeendelea kutoa elimu kwa umma ili kila mkazi wa Wilaya hii ajue haki zake za msingi, aichukie rushwa na awe mstari wa mbele kutoa ushirikiano wa kuwafichua wenye tabia ya kutoa na kupokea rushwa.

Vilabu vya wapinga Rushwa (**Anti Corruption Clubs**) vimeanzishwa katika shule za Msingi Sekondari na Vyuo vilivyopo Wilaya ya Kigamboni. Ugawaji na usambazaji wa vipeperushi na majarida umefanyika kuelezea kuhusu madhara ya rushwa.

**Mheshimiwa Rais,**

Wilaya ya Kigamboni inatekeleza mikakati yakudhibiti ugonjwa wa Malaria kama ilivyoelekezwa na mpango wa Taifa wa kudhibiti Malaria nchini **(NMCP)**. Kwa mwaka **2016/2017** jumla ya wagonjwa waliolazwa kwa Malaria ni **102,503** kati ya **7,993** sawa na asilimia **8** ya wagonjwa wote waliolazwa katika vituo vyetu vya kutolea huduma za afya. Elimu ya kujikinga na maambukizi imekuwa ikitolewa kwenye jamii. Vyandarua 104,000 vyenye dawa vimegawiwa kwa kaya 43,208

**Mheshimiwa Rais,**

Ukimwi bado ni janga la kitaifa. Wilaya ya Kigamboni imeendelea kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi ya **UKIMWI/VVU** pamoja na ushauri nasaha na upimaji wa hiari. Kuanzia Januari hadi Desemba 2016, jumla ya watu **49,127** walijitokeza kwa hiari yao kupima virusi vya Ukimwi. Kati ya

hao **1,481** sawa na **3%** waligundulika kuwa na maambukizi ya virusi vya Ukimwi.

**Mheshimiwa Rais,**

Huduma za kuzuia maambukizi ya Ukimwi toka kwa mama kwenda kwa mtoto zinaendelea kutolewa. Kipindi cha Januari 2016 hadi Machi 2017, jumla ya wajawazito **7,039** walipimwa virusi vya **UKIMWI**. Kati yao **184** sawa na asilimia **3** ya waliopimwa walikutwa na maambukizi ya virusi vya **UKIMWI**. Aidha jumla ya watoto **3,172** walizaliwa. Kati yao watoto **6** sawa na asilimia **0.1** walikuwa na maambukizi ya Virusi vya **UKIMWI**. Vituo vya kutoa huduma ya kuzuia maambukizi toka kwa mama kwenda kwa mtoto vimeongezeka kutoka vituo **17** mwaka 2015 hadi **19** mwaka 2017.

**Mheshimiwa Rais,**

Wilaya ipo kwenye mapambano ya kutokomeza biashara na matumizi ya dawa za kulevya kuhakikisha kuwa hakuna kilimo wala biashara ya dawa hizo katika maeneo yetu. Aidha, serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali zikiwemo taasisi za **PILIMISANA FOUNDATION**, **PEDELEF** na **THE TIES** wanaendesha vituo vya kutoa huduma na kulea na kutoa elimu kwa vijana walioathirika na dawa za kulevya na kuzuia vijana wengine kujiingiza kwenye utumiaji wa dawa hizo.

**Mheshimiwa Rais,**

Leo Mwenge wa Uhuru umekimbizwa katika Kata **7.** Katika mbio hizo,jumla ya miradi **7** imekaguliwa, kuwekewa mawe ya msingi na kuzinduliwa. Miradi hii ina jumla ya thamani ya shilingi **229,422,929,552** ambapo serikali kuu imechangia shilingi **21,150,000,000,** Wahisani shilingi **95,000,000, Halmashauri shilingi 75,518,552** na Wananchi wamechangia shilingi **208,102,411,000.**

Miradi hii ipo katika sekta za viwanda, miundombinu, kilimo na uvuvi, afya, elimu na uwezeshaji kiuchumi **.(Kiambatisho II)**

**Mheshimiwa Rais,**
Mwenge wa Uhuru wa mwaka huu 2017 umebeba ujumbe usemao **"Shiriki kukuza uchumi wa viwanda kwa maendeleo ya nchi yetu"**, Ujumbe huu unaambatana na kauli mbiu za uhamasishaji jamii kama ifuatavyo:

1. **Mapambano dhidi ya Rushwa:** "Tuungane kwa pamoja dhidi ya rushwa kwa maendeleo,amani na usalama wa Taifa letu"
2. **Mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI:** "Tanzania bila maambukizi mapya; unyanyapaa na vifo vitokanavyo na ukimwi inawezekana".
3. **Mapambano dhidi ya dawa za Kulevya:** "Tujali na tuwasikilize watoto na vijana"
4. **Mapambano dhidi ya Malaria:** "Shiriki kutokomeza Malaria kabisa kwa manufaa ya jamii"

**Mheshimiwa Rais,**
Tunakuhakikishia kwamba ujumbe huo tumeupokea na tutautumia kuhamasisha wakazi wote wa Kigamboni kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya UKIMWI, Rushwa, Malaria na dawa za kulevya.

**Mheshimiwa Rais,**
Tunakutakia mafanikio katika uongozi wako, tupo pamoja nawe katika kusimamia kikamilifu juhudi za kujiletea maendeleo ili kuondokana na umaskini na kuinua uchumi wa nchi yetu.

Aidha, tunawatakia afya njema wewe na familia yako, hekima na busara. Mungu awape nguvu na uvumilivu na kuwa wenye maadili wakati wote wa mbio za Mwenge huku wakihamasisha shughuli za maendeleo nchini kote.

**MUNGU IBARIKI AFRIKA, MUNGU IBARIKI TANZANIA,**

Hashim Mgandilwa
**MKUU WA WILAYA**
**KIGAMBONI**